THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
CHUO CHA USIMAMIZI WA FEDHA
**THE INSTITUTE OF FINANCE MANAGEMENT**
(ESTABLISHED UNDER THE ACT No.3 OF 1972)

**9 Oktoba, 2025**

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA WA VITABU CHAKAVU

Wananchi wote mnatangaziwa kuwa Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM), Kampasi ya Dar es Salaam kitauza kwa njia ya mnada wa hadhara vitabu chakavu.

Mnada huo utafanyika siku ya **Ijumaa Tarehe 24 Oktoba 2025, saa nne asubuhi** katika eneo la maegesho ya magari ndani ya uzio wa Chuo cha Usimamizi wa Fedha, Barabara ya Shaaban Robert, Dar es Salaam.

### MASHARTI YA MNADA

1. Vitabu chakavu vitauzwa vilivyo na mahali vilipo;
2. Mnunuzi anatakiwa awe na vibali halali vya kukusanya na kusafirisha taka za karatasi zaidi ya tani tano vinavyotolewa na NEMC;
3. Mnunuzi atakayeshinda atatakiwa kuanisha eneo la urejelezaji analokusudia kupeleka. Eneo husika la urejelezaji linatakiwa liwe limefanyiwa tathmini ya athari kwa mazingira (EIA) na kupata Cheti cha EIA na vibali vingine vinavyo halalisha shughuli hizo sambamaba na kuwa na miundombinu inayokidhi mahitaji ya utekelezaji wa kazi hiyo;
4. Mmiliki wa kibali atakaye shinda anatakiwa kuwa na kitabu cha “Tracking Documents” kinachotolewa na Baraza (NEMC) ambacho kitatumika kwa ajili ya usafirishaji wa vitabu hivyo kutoka eneo la mnada hadi eneo la urejelezaji;
5. Vitabu chakavu ambavyo havitakuwa na sifa ya kurejelezwa vitatakiwa kuteketezwa kwa kuzingatia sheria na kanuni za mazingira;
6. Malipo ni asilimia mia moja (100%) na mteja atatakiwa kuondosha vitabu alivyonunua siku ya mnada;
7. Mnunuzi atakaye tamka bei ya juu na kushindwa kulipa, hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake kwa mujibu wa sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
8. Ruhusa ya kukagua vitabu chakavu itatolewa siku mbili kabla ya tarehe ya mnada; na
9. Vitabu hivyo ni kwa matumizi ya urejelezaji tu na haviruhusiwi kuuzwa madukani ajili ya matumizi ya Elimu ama matumizi mengine yoyote tofauti na urejelezaji.

Imetolewa na:

Prof. Jeremia Makindara
**Kny: MKUU WA CHUO**

*All correspondence should be addressed to the Rector*
5 Shaaban Robert Street, Post Code: 11101, P. O. Box 3918, Dar es Salaam – Tanzania,
Tel: **+255222112931-4**, **Fax: +255222112935**, **Email: rector@ifm.ac.tz**, **Website: www.ifm.ac.tz**

JIFUNZE UHUDUMIE